

## **1.0 UTANGULIZI**

### **1.1 UANDAAJI WA MPANGO MKAKATI**

Mpango Mkakati wa Halmashauri wa miaka mitano (2015 -2020) umeandaliwa kwa kufanya mapitio ya mpango uliokwisha muda wake (2008 -2012).

Msukumo wa kuandaa Mpango huu ultokana na sababu mbalimbali kama vile;

- Kutengwa kwa Wilaya ya Karagwe na kupata Wilaya mpya ya Kyerwa.
- Mahitaji ya utoaji huduma kwa wananchi.
- Mabadiliko ya Sera, Vipaumbele, Mipango ya Serikali.
- Hali halisi ya kiuchumi ya Wananchi.
- Ukuaji na ushirikishwaji wa Sekta binafsi.
- Umuhimu wa uwajibikaji wa Sekta ya Umma.

Mpango huu umeshirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo kuitia mikutano mbalimbali ya Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, Wadau wa maendeleo, Elimu na Afya ikiwa ni pamoja na Viongozi wa

Serikali, Wawakilishi wa wananchi, Taasisi za dini na mashirika binafsi.

Kuwepo kwa Mpango Mkakati huu kutawezesha Halmashauri kutoa huduma bora kwa jamii, kuongeza kipato kwa kaya, kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kuhakikisha ulinzi na usalama wa wananchi unaimarishwa ili kufikia malengo, Dhamira na Dira ya Halmashauri, MKUKUTA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

## **2.0 UCHAMBUZI WA HALI HALISI YA WILAYA**

### **2.1 HALI YA WILAYA**

#### **2.1.1 MIPAKA NA JIOGRAFIA**

Wilaya inapatikana kati ya nyuzi  $1^{\circ}$  na  $2^{\circ}$ ,  $20'$  Kusini Latitudo  $30^{\circ}$  hadi **38,30** Mashariki Longitudo.

Wilaya inapakana na Wilaya ya Kyerwa Kaskazini, Nchi ya Rwanda upande wa Kusini Magharibi, Wilaya ya Ngara upande wa Kusini na Wilaya ya Missenyi, Bukoba na Muleba upande wa Mashariki.

Wilaya ina eneo la kilomita za mraba **4,500**, kati ya kilomita za mraba **158** ni eneo la maji.

Mwinuko wa ardhi kutoka usawa wa bahari ni mita **1500** hadi mita **1800**. Hali ya hewa kwa ujumla ni joto la wastani wa  $26^{\circ}\text{C}$  ya kitropiki ambapo mvua hunyesha katika vipindi 2 vya msimu. Mvua

zinanyesha kwa wastani wa milimita 1,040 hadi 1,200 kwa mwaka kati ya mwezi Septemba na Januari na kati ya mwezi Machi na Mei. Sehemu kubwa ya Wilaya imezungukwa na safu za milima na mabonde. Hali ya hewa ya Uoto wa asili ni kisavana ambapo miti ya asili mbalimbali ipo katika miinuko na nyanda za chini.

### 2.1.2 IDADI YA WATU.

Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Karagwe ilikuwa na jumla ya watu **332, 020**. Kati ya hao **163,864** (wanaume) na **168,156** (wanawake), ambapo ongezeko la watu ni **2.9%** kwa mwaka. Maoteo ya watu kwa mwaka 2014 ni **351,556** Kati ya hao, wanawake ni **178,050** na wanaume ni **173,505**. Aidha idadi ya kaya nayo imeongezeka toka **72,836** hadi kaya **76,425**.

Msongamano wa watu katika kila kilomita moja ya mraba inakaliwa na watu **74** wakati wastani wa kitaifa ni **49**. Aidha idadi ya makundi mbalimbali ya kijamii ni watoto wenyе umri chini ya miaka 5 ambao idadi yao ni **60,445**, miaka 5 - 17 ni **116,691**, Vijana wenyе umri wa miaka 18 - 45 ni **116,652**, watu wenyе umri wa kuanzia miaka **46 - 59** ni **21,653** na wazee wenyе umri wa miaka **60** na kuendelea ni **16,579**. Pia Wilaya ina makundi mbalimbali ya watu wenyе ulemavu ambao ni walemvu wasioona **52**,

wasiosikia ni 16, wenyе ulemavu wa ngozi ni 22 na wenyе ulemavu wa viungo ni 1,237.

### **2.1.3UONGOZI NA UTAWALA.**

Wilaya ina Tarafa 5, Kata 23, Vijiji 76, Vitongoji 629 na jimbo moja la uchaguzi. Waheshimiwa Madiwani wa kuchaguliwa wapo 22 na kata moja mpya ya ishirini na tatu ambayo inatarajia kupata diwani katika uchaguzi Mkuu 2015. Waheshimiwa Madiwani wanawake viti maalum 7.

Wilaya inayo mamlaka ya Mji mdogo wa Kayanga. Mamlaka hii ina ukubwa wa mita za mraba 184, 500 na inaundwa na Tarafa moja ya Bugene yenye Kata tano za Ndama, Kayanga, Bugene, Nyakahanga na Ihanda zenyе vitongoji 35. Idadi ya wakazi kwa eneo la mamlaka ya mji mdogo ni 81,000 kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya 2012.

### **2.1.4 HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO YA WILAYA.**

Shughuli kuu ni kilimo cha kahawa kama zao la biashara, ndizi na maharage kama chakula na biashara na ufugaji hususani ng'ombe na mbuzi.

Mchango wa kila sekta katika maendeleo ya uchumi ni kilimo 80%, shughuli za biashara 5%, watumishi (kazi za ofisini) ni 3%, ufugaji 10%, na shughuli nyinginezo 3%. Pato la mwananchi kwa mwaka (Per-Capita Income) limeongezeka kutoka Tshs.

150,000/= kwa mwaka 2005 hadi kufikia Tshs.475,000/= kwa mwaka 2012 (Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi 2012). Na sasa linakadiriwa kufikia Tshs. 520,000 kwa mwaka 2015.

## 2.1.5 SHUGHULI ZA KIUCHUMI:

### 2.1.5.1 KILIMO, USHIRIKA NA UMWAGILIAJI:

Kilimo ni mojawapo ya shughuli za kiuchumi inayochangia wastani wa asilimia 70 ya pato la Halmashauri. Kaya zinazoshiriki katika shughuli za kilimo ni 61,351 kati ya kaya zote **76,425** za wilaya ya Karagwe. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 153,540 kati ya hekta 4,500,000 ya eneo lote la wilaya. Eneo linalofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji ni hekta 4,500 Pia Wilaya inashirikiana na wadau mbalimbali waliopo wilayani katika kuendeleza sekta ya kilimo. Baadhi ya wadau hao ni ELCT, Karagwe Agribusiness, MAVUNO, CHEMA, WORLD VISION, MATUNDA MEMA, BISHESHE WINE, KARAGWE ESTATE LTD, RADIO KARAGWE, RADIO FADECO, LUKALE WINE, KDCU, Matunda MEMA, KADERES NA OLAM.

Aidha zipo SACCOS 31 zenyе jumla ya wanachama 46,319 na Chama 1 kikuu cha Ushirika (KDCU) kinacho jishughulisha na ununuzi wa mazao ya wakulima. Wilaya imeanzisha na kujenga mradi mmoja mkubwa wa Umwagiliaji (Mwisa Irrigation

Scheme) wenyewe ukubwa wa Hekta 120. Uhamasishaji wa wananchi kulima mpunga na mbogamboga unaendelea. Mradi huu utaongeza kipato cha mkulima wa Karagwe na kupunguza umaskini.

#### **2.1.5.2 UFUGAJI NA UVUVI**

Wilaya ya Karagwe ina hekta 140,000 zinazofaa na hutumika kwa shughuli za ufugaji. Sekta hii uchangia kwa zaidi ya 10% katika ajira ya wananchi na pato la kaya. Mifugo ambayo hufugwa ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku, bata na sungura.

Shughuli za Uvubi ufanyika katika maziwa madogo ya Burigi, Rwakajunju, Kamakala na mto Kagera. Wilaya inayo mabwawa ya kuchimbwa 67 kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Uzalishaji wa samaki ni wastani wa kilo 33,000 kwa mwaka. Aina za samaki wanaozalishwa kwa wingi ni sato/ngege, kambale mamba, kambale mumi, furu, ningu, soga na domodomo.

#### **2.1.5.3 VIWANDA NA BIASHARA**

Mji wa Kayanga na Omurushaka pamoja na miji midogo ya Kihanga, Nyakaiga, Rwambaizi, Nyaishozi, Chanyamisa, Nyabiyonza, Nyakabanga na Ihembe ni kati ya miji inayokua kibashara na yenye mwingiliano mkubwa wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Maeneo haya yanaendelea

kuwekeza katika viwanda vya biashara kama vile viwanda vya kukoboa Kahawa, viwanda vya kusindika maziwa, asali, kusaga na kukoboa nafaka. Shughuli za uzalishaji zinaendelea kuimarika na kuongeza uzalishaji, kupanua ajira, kukuza biashara ya uuzaji na ununuzi wa mazao tarajiwa na hivyo kuongeza kipato na kukuza uchumi, kuboresha maisha ya jamii, kupunguza umaskini wa kipato na hivyo kuchochea kasi ya kuondoa umaskini.

## **2.1.6 HUDUMA ZA KIJAMII**

### **2.1.6.1 NISHATI YA UMEME.**

Huduma ya umeme inapatikana wilayani na idadi ya watumiaji **5,989** wananaufaika na huduma hii katika vijiji 77. Huduma hii inatolewa na shirika la umeme Tanzania (TANESCO). Kuwepo kwa huduma hii kumechangia kuwepo kwa ongezeko la shughuli za kiuchumi kama vile Biasharana viwanda vidogo vidogo.

### **2.1.6.2 SIMU.**

Huduma za simu za mkononi zinatolewa na makampuni ya TTCL, Tigo, Vodacom, Airtel na Zantel, na kurahisisha mawasiliano na ukuaji wa uchumi. Pia ipo huduma ya mtandao wa internet ”.

### **2.1.6.3 POSTA.**

Huduma za Posta zinapatikana katika kata za Kayanga, Nyakasimbi, Kanoni, na Bugene. Shirika pia linatoa huduma ya kutuma pesa kwa haraka kupitia "Electronic Money Order" na kutuma pesa nje ya nchi kwa njia ya "Western Union Money Transfer". Aidha vifurushi vya "EMS" vimeingizwa kwenye mtandao pamoja na Uwakala wa huduma za M-pesa na LUKU.

### **2.1.6.4 HUDUMA ZA KIFEDHA/BENKI.**

Zipo benki 3 za CRDB, NMB na Benki ya Posta, ambazo zinatoa huduma nyingine za kibenki kwa wateja ikiwemo mikopo kwa wafanyakazi na wajasiriamali. Pia Benki hizi hutoa huduma kupitia mitandao ya simu za mkononi na ATM. Zipo taasisi zinazotoa huduma za kifedha kwa wananchi kama vile Bayport, Pride (T), Vision Fund, na SACCOS kama vile KAWOSA, WAESA, TUWAKA na UVIKASA

### **2.1.6.5 HUDUMA YA ELIMU**

Wilaya inayo madarasa ya Elimu ya Awali 108 kati ya madarasa 110 yanayohitajika. Shule za msingi zilizopo ni 117 kati ya hizo za serikali ni 110 na zisizo za serikali 7. Wilaya ina jumla ya shule za Sekondari 25 zenye jumla ya wanafunzi 9,064 kati yao 4,330 wakiwa ni wavulana na 4, 734 ni wasichana.

## 2.1.6.6 HUDUMA ZA AFYA

Idara ya Afya imeendelea kutekeleza mpango wa utoaji huduma mbalimbali za Afya kwa kupitia vitengo vyake katika vituo vyote vya tiba 41. Katika vituo vya tiba vilivyopo **36** vinamilikiwa na Serikali na vituo **5** ni vya watu binafsi na mashirika ya dini.

## 2.1.6.7 HUDUMA YA MAJI

Huduma ya Maji Mjini inatolewa na Mamlaka ya Maji Mjini Karagwe tangu mwaka 2004. Uzalishaji maji mjini kwa sasa ni wastani wa mita za ujazo 246 kwa siku wakati mahitaji ni mita za ujazo 2,006 kwa siku.

Idadi ya wakazi wanaopata maji safi na salama vijijini ni asilimia **48** ikilinganishwa na wastani wa asilimia **56.9** ya upatikanaji wa maji kitaifa. Miundombinu ya maji iliyopo ni kama ifuatavyo;

*Jedwali Namba 1: Mindombinu ya Maji Wilayani Karagwe*

Na	Aina ya Mradi	Idadi
1	Maji bubujiko (Gravity scheme)	18
2	Miradi inayotumia nguvu za mashine	10
3	Visima virefu	71
4	Visima vifupi	50
5	Vyanzo vilivyoboreshw	86
6	Uvunaji wa maji a mvua	593

## 2.1.6.8 MIUNDOMBINU YA BARABARA.

Wilaya ya Karagwe mpaka kufikia Desemba, 2014 kuna mtandao wa barabara zenyé urefu wa km.1, 816.7 ambao kati ya hizo km. **263** ni za Mkoa, km. **1386.7** ni za Wilaya na km. **214** ni za Vijiji. Kati ya kilomita hizo km. **51** ni barabara za lami za mkoa na km. **4** barabara ya lami za Wilaya. **Kilomita 682** ni za Changarawe na **km.1079.7** ni za udongo na zinapitika kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

## **2.2 UCHAMBUZI WA MAZINGIRA**

Uchambuzi huu wa mazingira umezingatia mapendekezo na mapitio ya makundi na taasisi tofauti ambazo kuwepo kwao kunaweza kuathiri maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya Karagwe. Uchambuzi huu umewezesha Halmashauri kutambua wadau wake na mahitaji yao. Pia uchambuzi umewezesha kupatikana kwa mambo ya msingi ambayo yanaeleza vizuri uwezo, mapungufu, fursa na changamoto kwenye utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Halmashauri ya Wilaya Karagwe.

### **2.2.1 UCHAMBUZI NA UAINISHAJI WA WADAU WA MAENDELEO**

Utambuzi wa wadau wa Maendeleo katika halmashauri ya wilaya Karagwe ni muhimu ili kutambua michango yao kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Lengo la utambuzi huu ni kutambua majukumu na matarajio yao. Matarajio ya wadau ni kupata ushirikiano mzuri na sekta ya umma. Uchambuzi wa wadau ulifanyika ili kubaini malengo muhimu ya kushughulikia katika kutatua changamoto na vikwazo vya maendeleo na kuainisha vipaumbele, viwezeshi pamoja na fursa zilizopo za maendeleo.

*Jedwali Namba 2: Uchambuzi wa Wadau wa Maendeleo*

<b>Na.</b>	<b>Wadau</b>	<b>Matarajio</b>	<b>Vikwazo na changamoto katika kufikia Matarajio.</b>	<b>Ulinganisho wa umuhimu K, W na N.</b>
1.	Serikali za Vijiji	<p>Kuwezesha upatikanaji wa sera na miongozo ya kiutawala katika;</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Uongozi na masuala ya kifedha</li> <li>⇒ Uchambuzi wa Mipango ya kiuchumi</li> <li>⇒ Mafunzo.</li> <li>⇒ Masuala ya kisheria</li> <li>⇒ Maendeleo ya kijamii</li> </ul> <p>Maelekezo ya kisera na mipango ya maendeleo ya kisekta;</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Kilimo</li> <li>⇒ Ushirika</li> <li>⇒ Mifugo</li> <li>⇒ Viwanda na Biashara</li> <li>⇒ Maliasili</li> </ul> <p>Maelekezo ya kisera na huduma za kijamii</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Elimu</li> <li>⇒ Afya</li> <li>⇒ Upatikanaji wa maji</li> <li>⇒ Ustawi wa jamii.</li> </ul> <p>Mipango halisi ya maendeleo na huduma</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Uwezo mdogo wa kitaalamu katika kusimamia na kutekeleza mipango ya Halmashauri</li> <li>⇒ Ushirikishwaji hafifu wa mipango ya maendeleo ya vijiji.</li> <li>⇒ Ukiukwaji wa ilani ya uchaguzi na misingi ya utawala bora.</li> <li>⇒ Usimamizi mbovu wa shughuli za maendeleo za vijiji</li> <li>⇒ Ukosefu wa ajira</li> <li>⇒ Upungufu wa chakula.</li> <li>⇒ Ongezeko la umaskini</li> <li>⇒ Uharibifu wa mazingira</li> <li>⇒ Uzalishaji hafifu katika shughuli za kilimo.</li> <li>⇒ Elimu duni, Afya na ustawi wa jamii.</li> <li>⇒ Milipuko ya magonjwa</li> <li>⇒ Uzalishaji hafifu katika sekta muhimu za kiuchumi na kijamii.</li> <li>⇒ Ongezeko kubwa la vitendo vya uvunjifu wa amani na matatizo ya kijamii (watoto wa</li> </ul>	K

		<p>za kiuhandisi:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Usanifu wa kitaalamu katika ujenzi wa majengo/miundombi nu, zabuni na mikataba ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>mitaani,ulevi,madawa ya kulevyo n.k)</li> <li>⇒ Mipango duni ya makazi ya watu</li> <li>⇒ Upungufu wa miundombinu mbalimbali katika Wilaya</li> <li>⇒ Ongezeko la majanga kama vilemoto,njaa,ukame,kimbunga n.k</li> <li>⇒ Upungufu na ubovu wa miundombinu ya usafirishaji na ongezeko la ajali.</li> </ul>	
2.	Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) na Kijamii (CBOs)	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Wadau katika mchakato wa maendeleo.</li> <li>⇒ Ushirikishwaji katika sera za maendeleo</li> <li>⇒ Kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha sekta binafsi kufanya kazi kwa ufanisi</li> <li>⇒ Utawala bora na uvezeshi</li> <li>⇒ Kuimarisha uwezo wa NGOs and CBOs ili kuhakikisha majukumu yao yanatekelezwa ipasavyo</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Gharama kubwa kwa serikali kutekeleza shughuli ambazo NGOs na CBOs wana uwezo wa kuzitekeleza</li> <li>⇒ Kutozingatia sheria zinazoongoza shughuli za NGOs na CBOs</li> <li>⇒ Uratibu hafifu wa shughuli maendeleo ya NGOs na CBOs</li> <li>⇒ Ushindani kati ya NGOs na CBOs</li> </ul>	K

3.	Taasisi za dini	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Ushirikishwaji katika mipango ya maendeleo.</li> <li>⇒ Ushirikishwaji katika uandaaji wa sera za maendeleo na huduma za jamii</li> <li>⇒ Kuimarisha uwazi, uwajibikaji na uvezeshikati ya taasisi za dini, serikali na wadau mbalimbali</li> <li>⇒ Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za dini, serikali, wafadhili na wadau</li> <li>⇒ Kuiwezesha upashanaji taarifa ili kuwa na matumizi bora ya rasilimali na kubadilishana uzoefu</li> <li>⇒ Kuwepo na amani, utii wa sheria na mamlaka.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Uratibu hafifu wa shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma za kijamii</li> <li>⇒ Ongezeko la uharifu na matatizo ya kijamii</li> <li>⇒ Ushindani kati ya taasisi za kidini na matumizi ya rushwa na kutozingatia haki za binadamu katika utoaji wa huduma za kijamii</li> <li>⇒ Mtiririko mbovu wa taarifa kutoka katika taasisi moja na nyingine.</li> <li>⇒ Mahusiano ya kusuasua kati ya Serikali, Wadau wengine wa maendeleo na mashirika ya dini</li> <li>⇒ Ukosefu wa ubunifu katika kutoa huduma kwa jamii.</li> </ul>	K
----	-----------------	---	---	---

4.	<p>Mashirika na taasisi za umma (TANESCO, TTCL, NMB, CRDB, KDCU, TRA, NSSF, LAPF, PSPF and NIC).</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Kuwezesha ubadilishanaji na upatikanaji wa taarifa katika kutumia raslimali na utaalamu</li> <li>⇒ Kuimarisha mbinu za kushirikiana.</li> <li>⇒ Kuimarisha hifadhi ya jamii na misingi ya kisheria pamoja na amani</li> <li>⇒ Kutoa huduma za kiuchumi na kijamii katika jamii na mashirika mbalimbali.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Ushirikiano hafifu kati ya Mashirika ya umma na mamlaka ya Serikali za mitaa</li> <li>⇒ Mbinu hafifu za kufuatilia miradi ya maendeleo.</li> <li>⇒ Ongezeko la vitendo viovu na uvunjifu wa amani.</li> <li>⇒ Utoaji wa huduma hafifu na watu kutojamini.</li> </ul>	K
5.	<p>Sekta binafsi na TCCIA</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Miongozo ya kisera.</li> <li>⇒ Uwazi na ugatuaji</li> <li>⇒ Uthibiti wa ubora.</li> <li>⇒ Uhamasishaji wa sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za uchumi.</li> <li>⇒ Kutoa maelekezo na ufanuzi juu ya sera ya uwekezaji na kuitia sheria za uwekezaji wa biashara.</li> <li>⇒ Kupitia na kuhamasisha sera za biashara ya ndani, na biashara ya kimataifa.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>⇒ Rushwa.</li> <li>⇒ Ukiritimba.</li> <li>⇒ Mawasiliano hafifu kati ya Halmashauri na sekta binafsi.</li> <li>⇒ Kukwepa ulipaji wa kodi</li> <li>⇒ Increased poverty.</li> <li>⇒ Ukosefu wa ajira.</li> <li>⇒ Kushuka kwa uchumi.</li> <li>⇒ Uhaba wa huduma za jamii.</li> </ul>	K

		⇒ Kuendelea kushirikiana na asasi nyingine binafsi.		
6.	Vyama vya Siasa	<p>⇒ Utekelezaji wa sera za chama Tawala.</p> <p>⇒ Tathmini ya sera</p> <p>⇒ Mshindo nyuma wa kisera.</p> <p>⇒ Utawala bora.</p>	<p>⇒ Kukwamisha vipaumbele vya halmashauri kufanikiwa.</p> <p>⇒ Viongozi wa siasa kutosaidia Serikali za Vijiji, Halmashauri na Kamati za kudumu</p> <p>⇒ Uchangiaji hafifu wa wananchi katika maendeleo.</p> <p>⇒ Mawasiliano hafifu kutoka katika ngazi za chini hadi Halmashauri.</p> <p>⇒ Ukosefu wa nguvu ya mamlaka katika kutatua matatizo ya kisiasa.</p>	K
7.	Watumishi wa Halmashauri	<p>⇒ Kusahihisha na kutafsiri sera mbalimbali.</p> <p>⇒ Fursa kwa shughuli za uzalishaji katika kukuza uchumi na masoko ya mazao yao.</p> <p>⇒ Masuala ya jinsi na rika</p> <p>⇒ Fursa katika ajira</p>	<p>⇒ Rushwa</p> <p>⇒ Ukiritimba</p> <p>⇒ Utoaji wa huduma duni</p> <p>⇒ Ukosefu wa ajira</p>	K
8.	Watoto wenyе umri wa kwenda shule (Wavulana na Wasichana).	<p>⇒ Fursa sawa katika kupata elimu bora.</p> <p>⇒ Fursa ya kupata matibabu na lishe bora</p>	<p>⇒ Upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia</p> <p>⇒ Upungufu wa huduma za jamii.</p> <p>⇒ Upungufu wa Walimu</p>	W

9.	Watoto chini ya umri wa miaka 5	⇒ Fursa ya kupata matibabu na lishe bora	⇒ Upungufu wa madawa katika vituo vya tiba na miundombinu michache.	W
10.	Wanawake wajawazito	⇒ Fursa ya kupata huduma za bora za kliniki na matibabu	⇒ Huduma duni katika vituo vya tiba	W
11	Wakulima,Wa fugaji na Wavuvi	⇒ Fursa ya kupata huduma za maafisa ugani katika maeneo yao. ⇒ Soko la uhakika la samaki	⇒ Huduma duni za ugani	K
12	Watu wenye ulemavu	⇒ Upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi	⇒ Mipango duni isiyozingatia matakwa ya watoto wenye ulemavu.	W
13	Vikundi vya uzalishaji	⇒ Mipango yenye kuzingatia jinsia ⇒ Fursa ya kupata ajira ⇒ Fursa kwa shughuli za uzalishaji katika kukuza uchumi na masoko ya mazao yao	⇒ Huduma duni za ugani	K
14	Wanasiasa/M adiwani	⇒ Mazingira wezeshi katika kutenda kazi kwa watumishi ⇒ Ulinzi na usalama ⇒ Mipango yenye kuzingatia jinsia	⇒ Ushirikiano hafifu katika kusimamia sera ⇒ Mbinu duni za kutathmini sera	W
15	Wizara (OWM –TAMISEMI) na Wizara nyingine za	⇒ Usimamizi, Sera, Miongozo na mrejesho nyuma na Uwezeshaji	⇒ Ushirikiano hafifu kati ya Wizara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. ⇒ Migogoro na utendaji	K

	kisekta		duni wa kazi	
16	Wafadhili	⇒ Fedha ⇒ Ushauri katika Miradi ⇒ Usimamizi na Ufuatiliaji	⇒ Ushirikiano duni. ⇒ Migogoro na utendaji duni wa kazi.	K
17	Wilaya jirani	⇒ Wauhishaji ⇒ Wafuatiliaji	⇒ Ushirikiano duni. ⇒ Migogoro na utendaji duni wa kazi	W

Zingatia; K – Umuhimu Mkubwa

W –Umuhimu wa Kati

N – Umuhimu Kidogo

## 2.2.2 UCHAMBUZI WA UWEZO, UDHAIFU, FURSA NA VITISHO

Uchambuzi huu ulizingatia zaidi masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na mazingira ya teknolojia iliyopo kwa sasa. Matokeo ya uchambuzi yalikuwa kama ifuatavyo:

### 2.2.2.1 Uwezo (Strengths)

- Asilimia 80 ya wakazi inajihusisha na shughuli za kilimo.
- Asilimia 52 ya ardhi inayoweza kulimwa haijatumika kwa kilimo.
- Mtando mzuri wa barabara za Wilaya na za vijiji.
- Wilaya inazo raslimali nyingi za maziwa, mito, hifadhi za wanyama pori, misitu na ardhi.
- Kuwepo kwa utulivu na amani.
- Ushirikiano Imara baina ya viongozi wa Wilaya.
- Uwepo wa Wakuu wa Idara wenye sifa.
- Uwepo wa taasisi zinazotoa huduma za kijamii mpaka ngazi ya vijiji.

- Eneo la utawala na ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo linafikika zaidi

#### **2.2.2.2 Fursa (Opportunities)**

- Kuwepo kwa wadau wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Barabara za Mkoa na Taifa zinazopitika kipindi chote cha mwaka kwa 90% huchangia kurahisisha usafiri na usafirishaji.
- Hali nzuri ya hewa ya Wilaya na uwepo wa rasilimali za asili inaruhusu uwekezaji kwenye kilimo na mifugo
- Kuwepo mitandao ya mawasiliano kwa muda wote
- Upatikanaji wa umeme wa uhakika mpaka vijijini

#### **2.2.2.3 Udhaifu (Weaknesses)**

- Uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo na mifugo.
- Uharibifu wa mazingira.
- Uhaba wa masoko.
- Masharti magumu ya mikopo, kwenye taasisi za kifedha
- Mila na desturi potofu.
- Uhaba wa rasilimali watu na upungufu wa rasilimali fedha.
- Kutofuata mpango bora wa matumizi ya ardhi
- Ushiriki hafifu wa jamii kwenye shughuli za maendeleo
- Mwitikio hafifu katika usimamizi wa sheria

#### **2.2.2.4 Vitishio/Vikwazo (Threats)**

- Madhara ya UKIMWI/VVU dhidi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuongezeka kwa kiwango cha watu wasio na ajira
- Utashi wa kisiasa

- Mabadiliko ya tabia ya nchi

### 2.2.3 MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA

Halmashauri ya Wilaya Karagwe imebaini mambo na maeneo muhimu ya kuzingatia ili kuweza kufikia kiwango tarajiwa cha ukuaji wa uchumi;

- Ushirikishwaji wa jamii katika kufanya maamuzi ya maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.
- Uzingatiaji wa masuala ya usawa kijinsia
- Uwajibikaji, uwazi na uadilifu kwenye usimamizi wa masuala ya umma
- Elimu kwa jamii kuhusu fursa zilizopo Wilayani ili waweze kuboresha mazao ya kilimo na mifugo
- Uwepo wa Amani na Usalama Wilayani
- Mapambano dhidi ya ongezeko la maambukizi ya HIV/AIDS na kutoa misaada kwa watoto walio kwenye mazingira magumu
- Ushiriki wa wadau kikamilifu kwenye uibuaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya usimamizi wa mazingira.

### **3.0 DIRA NA DHAMIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE:**

Dira inafafanua hali au kiwango kinachotegemewa na Halmashauri (wanajamii wa Karagwe) kwa kipindi cha miaka ya mbele ijayo, Dhamira inafafanua mwelekeo wa shughuli za Halmashauri na viwango vitakavyofikiwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe baada ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa shughuli zilizotekelawa kwa Dira na Dhamira zilizokuwepo imebaini, kauli zote mbili (Dira na Dhamira) bado zinaendana na Dira ya Taifa ya 2025

#### **3.1 *Dira:***

***Kuwa na Jamii inayowajibika kwa maendeleo yake, maisha bora, uchumi endelevu, huduma bora za kijamii na Amani.***

#### **3.2. *Dhamira***

***Kujenga uwezo Na kuiwezesha jamii Kwa kushirikisha wadau wote katika kuamua, kupanga na kutekeleza vichocheo vyta maendeleo ili raslimali zilizopo zitumike kwa usahihii na kwa kuzingatia kanuni ya uwazi na uwajibikaji.***

Katika kuhakikisha kwamba Dira na Dhamira ya Halmashauri inafikiwa maeneo ya msingi yafuatayo yalizingatiwa;

- Uboreshaji wa kiwango cha maisha ya wananchi.
- Uzingatiaji wa utawala bora na utawala wa sheria.
- Uendelezaji wa uchumi endelevu sanjari na sera na mipango ya Taifa.
- Kwa kuzingatia wajibu wa Halmashauri ya Wilaya, katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi, umeandaliwa muundo utakaozingatia yafuatayo:

- Kuwa na utaratibu uliowazi katika kuthibiti masuala yanayohusiana na vitendo vya rushwa
- Kuwepo kwa utoaji huduma wa kiuchumi na kijamii unaokidhi kiwango.
- Kuwepo kwa mfumo bora wa upashanaji habari baina ya viongozi, watendaji na wananchi.
- Kuhakikisha maamuzi yanafikiwa kwa njia ya kidemokrasia.
- Kuhakikisha mgawanyo na usimamizi wa raslimali fedha katika shughuli za maendeleo.
- Kuzingatia uthibiti wa matumizi ya fedha za Halmashauri.
- Kukubali mabadiliko kila inapobidi.
- Kuwepo kwa ushirikiano wa kutosha baina ya watendaji.
- Kuwepo kwa uwazi katika taratibu za kugawa madaraka na kudhibiti kiwango cha ufanisi.

#### **4.0 MAENEO MUHIMU YA MATOKEO YANAYOTEGEMEWA KATIKA MPANGO**

Mpango mkakati huu umebaini maeneo muhimu ya matokeo yanayotegemewa kama ifuatavyo;

- Kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya UKIMWI/VVU
- Kuinua kiwango cha maisha ya wananchi hususani katika kuondoa umaskini.
- Kuwashirikisha wananchi katika kuamua na kutekeleza shughuli zao za maendeleo.
- Uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika jamii.
- Uhifadhi wa mazingira.
- Matumizi sahihi na yenye ufanisi wa raslimali za Halmashauri katika utoaji huduma.
- Uwazi na uwajibikaji katika shughuli za Halmashauri kwa wananchi.

## **5.0 MPANGO MKAKATI WA WILAYA YA KARAGWE KWA MWAKA 2015 - 2020:**

Sehemu hii inazo safu ndogo kuu nne zenyе ufanuzi mbali mbali. Safu hizo ni Lengo mahsusи, Mikakati, Shughuli na Viashiria vya Mafanikio.

➤ **Lengo Mahsusи:**

Sehemu hii inaonesha malengo mahsusи ya kutekelezwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo, hivyo sehemu hii ni mhimili mkuu katika kufikia maeneo muhimu ya matokeo.

➤ **Mikakati:** Sehemu hii inaonesha mpangilio wa mambo ya kufanyika kufikia malengo mahsusи.

➤ **Shughuli:** Sehemu hii inaonesha kazi zitakazofanyika katika kutekeleza mkakati husika.

➤ **Viashiria vya mafanikio:** Sehemu hii inaonesha kigezo cha kuona matokeo ni kwa jinsi gani lengo mahsusи limefikiwa.

Majedwali yafuatayo kuanzia jedwali namba 3 hadi 8 yanaonyesha uchambuzi wa kina wa malengo makuu, malengo mahsusи, mikakati, shughuli zitazofanyika na viashiria vya mafanikio ya Mpango Mkakati

**JEDWALI NAMBA 3**

**LENGO MUHIMU LA MATOKEO NA.1 : UBORESHAJI WA HUDUMA NA KUPUNGUA MAAMBUKIZI YA UKIMWI**

LENGO MAHSUSI	MIKAKATI	SHUGHULI	VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI
1.1 Kupungua maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka asilimia 5.8 hadi asilimia 2 kufikia mwaka 2020.	1.1.1 Kuhamasisha wafanyakazi na jamii kwa ujumla kutambua madhara ya UKIMWI/VVU na jinsi ya kujikinga.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuendesha semina kwa watumishi wa Afya 120 juu ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT Option B+)</li> <li>➤ Kuhamasisha watumishi 4000 na jamii juu ya upimaji wa hiari katika kata 23.</li> <li>➤ Kununua na kusambaza kondomu katika kata 23 kwenye nyumba za kulala wageni, vituo vya Afya na mahali pa kazi.</li> <li>➤ Kuongeza na kuboresha huduma za PMTCT na ushauri nasaha kwenye vituo 40 vya tiba.</li> <li>➤ Kuendesha semina kwa vikundi vya vijana 189 katika vijiji 77 na Vitongoji vya mji mdogo 35 juu ya stadi za maisha.</li> <li>➤ Kuendesha semina kwa walimu 284 juu ya kubadili tabia, kutoka shule142 (wawili wawili kila shule)</li> <li>➤ Kuendesha semina kwa makundi yanayoishi katika mazingira</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Maambuki zi ya virusi vya UKIMWI kupungua kwa asilimia 3.8</li> </ul>

		<p>hatarishi juu ya kujikinga na maambukizi ya Ukimwi (Wavuvi 300, wahudumu wa baa 100, madereva 100, wafungwa 200, polisi 60, watumishi Ugani 100 na Saloon (wanawake na wanaume).</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kushirikiana na viongozi wa Taasisi mbali mbali 100 za Dini, Azise, CBO, FBO kutoa elimu juu ya kubadili tabia kwa wafuasi wao na wateja wao.</li> <li>➤ Kusambaza makala na vipeperushi na kuelimisha jamii kwa ujumla kupitia vyombo vyta habari na cinema katika vijiji 77 na vitongoji vya mji mdogo 35.</li> <li>➤ Kuimarisha sheria ndogo za vijiji kudhibiti ulevi wa kupindukia na sherehe za usiku, na kuanzisha sheria ndogo ya kudhibiti maambukizi ya UKIMWI/VVU, katika vijiji 77 na vitongoji vya mji mdogo 35.</li> </ul>	
		<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuendesha kampeni juu ya tohara kwa wanaume kati ya miaka 15-49 katika kata zote 23.</li> </ul>	
	1.1.2 Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango inayolenga kupunguza ukali wa	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kusambaza dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs) na dawa za kifua kikuu (TB) kwa waathirika</li> </ul>	

	madhara yanayotokana na UKIMWI/VVU.	<p>6000 kila mwaka.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuwagawia vyakula vyenye mlo kamili na vifaa vingine vya kusaidia watumishi waathirika 100 wanaoishi na UKIMWI.</li> <li>➤ Kutoa fedha/mikopo ya mzunguko kwa ajili ya miradi ya uzalishaji mali kwa vikundi vya waathirika 1,500.</li> <li>➤ Kuwalipia karo na vifaa vingine vya shule watoto 2,600 wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kila mwaka.</li> <li>➤ Kulipia gharama za matibabu kwa kaya 4000 zinazolea yatima kila mwaka.</li> <li>➤ Kubaini watoto yatima na kurekebisha takwimu zao katika vijiji 77 na vitongoji 35 vya mji mdogo</li> <li>➤ Kuendesha vikao vya kila robo mwaka kwa kamati za Kudhibiti UKIMWI za Wilaya, Kata na Vijiji.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii kupunguza unyanyapaa kwa waathirika wa UKIMWI katika kata 23.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii katika kusaidia watoto yatima na waathirika wa</li> </ul>
--	-------------------------------------	--

		UKIMWI kiuchumi na kijamii katika kata 23.	
		➤ Kutoa vifaa vya viwandani kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 20 za watoto yatima (watoto walezi wa wenzao).	
		➤ Kuendesha mikutano ya uhamasishaji juu ya mirathi na haki za binadamu katika kata 23.	

#### JEDWALI NA 4

#### LENGO MUHIMU LA MATOKEO NA. 2: KUINUA KIWANGO CHA MAISHA NA KUPUNGUZA UMASKINI

	LENGO MAHSUSI	MIKAKATI	SHUGHULI	VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI
2.1	Kuimarisha sekta binafsi kwa kuongeza fursa za ushiriki wa makundi ya wajasiriamali katika uzalishaji kutoka vikundi 114 hadi 214 ifikapo mwaka 2020	2.1.1 Kuhakikisha wahitimu kutoka vyuo vya ufundi, vijana, wanawake wajane, wazee pamoja na wasiojiweza wanaanzisha/wanajiunga katika vikundi vyta kibashara na ushirika.	➤ Kuhamasisha jamii kwenye Kata 23 hususani vijana na wanawake kijiungu na vyuo vya ufundi. ➤ Kutoa mafunzo ya ujasiliamali kwa vikundi 214. ➤ Kutoa mafunzo kwa wafanyabishara 750 juu ya kuongeza mitaji, usimamizi wa bishara, sheria na taratibu za bishara.	➤ Vikundi vya wajasiriamali 100 vimesajiliwa
2.2	Kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 3.3 hadi tani 17 ifikapo 2020.	2.2.1 Kulinda mazilio ya samaki yaliyopo.  2.2.2 Kuongeza mabwawa ya kuchimbwa kwa ajili ya ufugaji wa samaki kutoka 54 hadi 100.  2.2.3 Kuongeza vitendea kazi katika	➤ Kuhamasisha wanajamii katika vijiji 25 vinavyozunguka maeneo ya uvuvi kuhusu uvuvi endelevu.  ➤ Kuhamasisha wanajamii katika vijiji 20 kulinda mabwawa 21 yaliyopo na kuanzisha mengine mapya 79. ➤ Kununua boti ya kisasa kwa	➤ Ongezeko la uzalishaji wa samaki kwa tani 13.7

		shughuli za uvuvi.	ajili ya doria ili kuzuia uvuvi haramu.	
2.3	Kuungeza idadi ya vijiji vyenye mpango wa matumizi bora ya ardhi kutoka vijiji 21 hadi 77 ifikapo mwaka 2020.	2.3.1 Kushirikisha serikali za vijiji na jamii katika kuweka mipaka ya ardhi.  2.3.2 Kuhakikisha kila kijiji kina mpango bora na masjara ya ardhi.	➤ Kuelimisha kamati 30 za vijiji kuhusu matumizi bora ya ardhi na usimamizi wake.  ➤ Kuviwekea vijiji mipaka ya mashamba kwa kaya 50,000 na Kutoa hati za kimila za kumiliki ardhi  ➤ Kutoa mafunzo kwa viongozi wa vijiji 77 juu ya uandaaji na utumiaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi.	➤ Ongezeko la Vijiji 56 vyenye mpango wa matumizi bora ya Ardhi
2.4	Kuboresha usimamizi na kuungeza idadi ya vyama vya ushirika vilivyosajiliwa kutoka 31 hadi 51 kwa mwaka 2020	2.4.1 Kuhakikisha vikundi vya kiuchumi vya vijana na wanawake vinaanzisha vyama vya ushirika na kusajiriwa  2.4.2 Kujenga uelewa wa kanuni za ushirika.	➤ Kuhamasisha vikundi 40 vya kuweka na kukopa vya wafugaji na wavuvi juu ya taratibu za usajili.  ➤ Kuendesha mikutano kwenye vijiji 77 juu ya usimamizi wa SACCOS na AMCOS. ➤ Kutoa mafunzo kwa viongozi wa SACCOS na AMCOS juu ya sheria ndogo na miongozo, uendeshaji na usimamizi wa ushirika	➤ Vyama vya ushirika 20 vya kuweka na kukopa vilivyosajiliwa ➤ Idadi ya vyama vya ushirika vilivyo hai
2.5	Kuboresha mtandao wa barabara zenyetilizwa kilometa 1,553.1 ziweze kuitika mwaka mzima kufikia 2020.	2.5.1 Kubaini maeneo ya kufanyiwa ukarabati na kutunza mtandao wa barabara.  2.5.2 Kuhakikisha ukarabati wa barabara wa mara kwa mara	➤ Kufanya matengenezo ya kawaida, maalum na korofi kwa km 1,553.1  ➤ Kuanzisha mtandao wa barabara za lami km 20 ➤ Ujenzi wa madaraja na kalvati 115	➤ Kilometra 1,553.1 zimefanyiwa matengenezo

		unafanyika  2.5.3 Kuhakiksha ujezi wa miundombinu ya barabara inatekelezwa	➤ Kuhakikisha uratibu, usimamizi na ufuatiliaji unafanyika	
2.6	Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa 60% ifikapo 2020.	<p><b>2.6.1</b> Kuhakikisha wakulima/wafugaji wanapata elimu juu ya uzalishaji bora wa kilimo/ mifugo.</p> <p><b>2.6.2</b> Kuhakikisha kunakuwepo na ufungaji bora wa kisasa.</p> <p><b>2.6.3</b> Kuhakikisha uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mazao na mifugo.</p> <p><b>2.6.4</b> Kuboresha hifadhi ya mazao kwa kujenga maghala 12 ili kupunguza upotevu wa mazao</p> <p><b>2.6.5</b> Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa ugani 62.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji 25,000.</li> <li>➤ Kuanzisha mashamba darasa (FFS) katika vijiji 77.</li> <li>➤ Kuanzisha vitalu 3 vya kuzalisha miche ya kahawa 1,000,000</li> <li>➤ Kuunda makundi ya wakulima/wafugaji katika vijiji 77.</li> <li>➤ Kutoa mafunzo kwa vikundi 150 vya wakulima juu ya kilimo biashara katika vijiji 77</li> </ul> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kununua vifaa na chanjo za mifugo</li> <li>➤ Kuzingatia sheria ndogo ndogo za kilimo/mifugo kuzuia uzururaji wa mifugo.</li> <li>➤ Kuboresha nyanda za malisho hekta 532</li> </ul> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kupata madume 60 bora ya ng'ombe na 50 ya mbuzi.</li> <li>➤ Kuanzisha na kuwezesha vikundi 120 vya wanyama wadogo</li> <li>➤ Kununua mbegu bora za mazao</li> <li>➤ Kutibu magonjwa yasababishwayo na kupe.</li> <li>➤ Ufuatiliaji na usimamizi wa</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Mazao ya kilimo na mifugo kuongezeka kwa asilimi 60.</li> </ul>

		2.6.6 Kupanua kilimo cha umwagiliaji kwa hekta 250	shughuli za kilimo na mifugo.	
2.7	Kupunguza magonjwa makuu:  Malaria toka 31.4 % hadi 10%.  Magonjwa ya moyo, kisukari na magonjwa ya kinywa na meno toka 6% hadi 2% Magonjwa ya maambukizi yatokanayo na maji machafu kupunguza toka 25% hadi 10% kwa mwaka 2020.	2.7.1 Kuhakikisha kuwa jamii inajengewa uwezo juu ya masuala ya afya na tiba  2.7.2 Kuimarisha/kuboresha huduma za kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza.  2.7.3 Kuwahuisha wadau wengine katika kupunguza magonjwa ya kuambukiza.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuanzisha skimu mpya 3 za umwagiliaji</li> <li>➤ Kutoa semina kwa tabibu 50 juu ya matibabu sahihi ya malaria.</li> <li>➤ Kutoa huduma ya tiba katika vituo vya serikali 32.</li> <li>➤ Kuanzisha huduma za matibabu ya kisukari na magonjwa ya moyo kwenye Hospitali 2 na Vituo vya Afya 2</li> <li>➤ Kuelimisha jamii juu ya kupata huduma ya magonjwa ya moyo na kisukari katika vituo 32 vya tiba.</li> <li>➤ Kuendesha warsha kwa watumishi 100 wa Afya juu ya Afya ya kinywa na meno.</li> <li>➤ Kuagiza na kununua vifaa na mashine ya matibabu ya kinywa na meno.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya Malaria kwa asilimia 21.4, Magonjwa kinywa na meno kwa asilimia 4, Magonjwa yatokanayo na maji machafu asilimia 15</li> </ul>
2.8	Kuboresha huduma za Afya na kupunguza vifo vya watoto wachanga toka 2/1000 hadi 1/1000 kufikia 2020.	2.8.1 Kuhamasisha jamii juu ya chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja.  2.8.2 Kuhakikisha kuwa huduma za Afya zinapatikana na kutolewa kwa jamii.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuwezesha upatikanaji wa chanjo kwa vituo vya tiba 57.</li> <li>➤ Kusambaza dawa na vifaa vya tiba mara moja kila mwezi.</li> <li>➤ Kusimamia na kufuutilia vituo 57 mara moja kila robo mwaka.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya chanjo za watoto kwenye vijiji 77 na Vitongoji 35 vya mji</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kiwango cha vifo cha watoto wachanga kushuka kwa asilimia 50</li> </ul>

			<p>mdogo.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ujenzi wa Hospitali 1 ya Wilaya na kuongeza vituo vya Afya 6 na zahanati 25</li> <li>➤ Kuongeza vituo vya huduma ya mkoba toka 109 hadi 140</li> </ul>	
2.9	Kupunguza vifo vya wajawazito kutoka 134/100,000 - 100/100,000 ifikapo 2020	2.9.1 Kuhamasisha jamii juu ya uzazi salama.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuhamasisha juu ya uzazi salama katika vijiji 77 na Vitongoji 35 vya mamlaka ya mji mdogo wa Kayanga.</li> </ul>	
		2.9.2 Kuboresha ujuzi wa watumishi wa Afya katika uzazi salama.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kubaini na kuendesha semina kwa walimu 20 wa ufundishaji kutoka vituo vya Tiba 53 juu ya uzazi salama.</li> <li>➤ Kutoa elimu ya uzazi salama kwa watumishi na wahudumu wa Afya 154.</li> <li>➤ Kutoa huduma ya uzazi wa mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu katika vituo vya tiba 33</li> </ul>	
		2.9.3 Kuboresha huduma za rufaa kwa wajawazito.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya uanzishaji wa mfuko wa huduma za rufaa katika kata 23</li> <li>➤ Kuanzisha mfuko wa mzunguko wa huduma za rufaa katika kila kituo cha tiba.</li> </ul>	
2.10	Kuboresha za Afya kwa wazee kutoka	2.10.1 Kuhakikisha wazee wote wanalipiwa bima ya Afya	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuwatambua wazee zaidi ya umri wa miaka 60 na kuwapatia</li> </ul>	Kuboreka kwa huduma za wazee

	asilimia 50 mpaka asilimia 95		<p>vitambulisho vya matibabu.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kusimamia huduma ya madirisha ya wazee katika vituo vyote vya tiba</li> </ul>	kwa asilimia 95.
2.11	Kuandaa michoro 10 ya mipango miji katika miji na vituo vya biashara 10 ifikapo mwaka 2020.	2.11.1 Kuhakikisha maeneo ya biashara yanapimwa ili kupunguza ujenzi holela.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kufanya mikutano 40 ya uhamasishaji kwa wakazi wa miji midogo ya biashara juu ya kupanga mji</li> <li>➤ Kuandaa michoro 10 ya mipango miji ya biashara na kuwasilisha michoro ili kupata kibali.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Idadi ya Michoro 10 ya mipango miji iliyotayarishwa na kupata kibali.</li> </ul>
2.12	Kuthamini majengo na viwanja vyote za Halmashauri kutoka 1% hadi 15% ifikapo 2020.	2.12.1 Kuhakikisha kuwa mali zote za halmashauri zinatathiminiwa na kupimwa na kupata hati milki	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kufanya uthamini ya majengo 100, viwanja 200 na mali nyingine za Halmashauri</li> <li>➤ Kufanya uthamini wa maeneo yasiyo pimwa ya miji ya Kayanga, Omurushaka na miji midogo 15.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Idadi ya Viwanja, majengo na mali nyingine zilizofanyiwa uthamini kuongezeka kwa asilimia 14.</li> </ul>
2.13	Kuungeza idadi ya viwanja vilivyopimwa mijini kutoka 500 hadi 1000 ifikapo 2020.	2.13.1kuhakikisha viwanja vya makazi na biashara vinapimwa na kupewa hati miliki	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kupima viwanja 500 mijini na kupatiwa hati miliki.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ongezeko la viwanja 500 vilivyopimwa</li> </ul>
2.14	Kuanzisha kamati za usimamizi wa wanyama pori toka kamati 6 hadi 10 kwenye vijiji vilivyo jirani na hifadhi za wanyama pori ifikapo mwaka 2020.	2.14.1 Udhibiti wa uvamizi wa wanyama pori katika maeneo ya makazi ya wananchi na raslimali zao.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuhamasisha jamii kuunda vikundi 10 shirkishi vya ulinzi wa jamii.</li> <li>➤ Kuratibu na kutambua ukanda salama (Buffer zone) 5 kati ya wanyama pori na wanavijiji.</li> <li>➤ Kuanzisha ‘game posts’ 4 kwenye vijiji 4</li> <li>➤ Kuendesha semina kwa viongozi wa vijiji 10 vinavyopakana na</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ongezeko la kamati 4 za usimamizi wa wanyama pori</li> </ul>

			hifadhi za wanyamapor.	
2.15	Kuboresha huduma za kielimu ifikapo mwaka 2020	<p>2.15.1 Kuhakikisha upatikanaji wa zana na vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi ili kuboresha kiwango cha elimu.</p> <p>2.15.2 kuhakikisha upatikanaji na ubora wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari</p> <p>2.15.3 kuhakikisha ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu kwenye chuo cha ualimu, sekondari na shule za msingi</p> <p>2.15.4 Kuongeza kiwango cha ufalu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa na kiwango cha usajili wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza.</p> <p>2.15.5 Kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati na bodi za shule</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuwezesha upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia (vitabu vya kiada na ziada) katika uwiano wa 1:1</li> <li>➤ Kuwajengea uwezo walimu 1,398 (mafunzo kazini)</li> <li>➤ Ujenzi wa madarasa 110 kwa shule za msingi na 38 shule za sekondari</li> <li>➤ Ujenzi wa nyumba za walimu 30 wa shule ya msingi na 10 kwa shule za sekondari</li> <li>➤ Upatikanaji wa madawati 1,000 kwa shule za msingi</li> <li>➤ Ujenzi wa mabweni 41 katika shule za sekondari</li> <li>➤ Ujenzi wa maktaba 10 katika shule za sekondari</li> <li>➤ Ujenzi wa matundu ya vyoo 500 kwa shule za msingi na 100 kwa sekondari</li> <li>➤ Ujenzi wa majengo ya utawala katika shule za sekondari 10</li> <li>➤ Ukamilishaji na ujenzi wa madarasa 6, mabweni 4, visima vya maji 3, jengo la utawala 1 na nyumba za watumishi 3 katika chuo/ sekondari</li> </ul>	Huduma za kielimu kuboreshwa

			<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ununuzi wa samani katika chuo/sekondari</li> <li>➤ Kuendesha semina kwa wajumbe wa kamati ba bodi za shule ili kutambua majukumu yao</li> <li>➤ Usimamizi na ufuatiliaji wa taaluma shulenii</li> </ul>	
2.16	Kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kutoka 10,000 hadi 4,000 ifikapo mwaka 2020.	<p>2.16.1 kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo kuhakikisha kuanzisha madarasa ya watu wazima.</p> <p>2.16.2 kufufua madarasa ya Elimu ya Watu Wazima (EWW)</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kutambua na kusajiri watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kwa njia ya 34ense katika vijiji 77 na vitongoji 35 katika mji mdogo.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa Elimu ya Watu Wazima katika vijiji 77 na vitongoji 35 vya mji mdogo.</li> <li>➤ Kuwajengea uwezo na kuingia mikataba walimu 212 wa EWW.</li> <li>➤ Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule 110</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kiwango cha watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kupungua kwa asilimia 40</li> </ul>
2.17	Kuboresha huduma ya maji kutoka asilimia 48 (2015) hadi 75 (2020)	Kusogeza huduma ya maji karibu na makazi ya watu	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kukamilisha miradi ya maji - program ya maendeleo ya awamu ya kwanza katika vijiji 5</li> <li>➤ Kuanza na kukamilisha miradi ya vijiji 10 awamu ya pili</li> <li>➤ Kujenga mradi wa maji toka ziwa Rwakajunju</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Upatikanaji wa huduma ya maji kuboreshwa kwa aslimia 27</li> </ul>

2.18	Kuinua kipato cha Wananchi wa Karagwe kwa kuimarisha shughuli za Ufugaji nyuki toka vikundi vya ufugaji nyuki 258 hadi vikundi 700	Kuhamasisha wananchi na sekta binafsi kujishughulisha na ufgaji wa nyuki	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kutengeneza na kusambaza mizinga 5,000 ya nyuki kwa vikundi 700 vya ufgaji nyuki</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuongezeka kwa Idadi ya vikundi vya ufgaji nyuki hadi 700 na uwepo wa mizinga 5,000</li> </ul>
------	--	--	--	---

**JEDWALI NAMBA 5**

**ENEO MUHIMU LA MATOKEO NA. 3: KUSHIRIKISHA JAMII KATIKA MAAMUZI YA SHUGHULI ZA MAENDELEO**

	LENGO MAHSUSI	MIKAKATI	SHUGHULI	VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI
3.1	Kuinua kiwango cha jamii katika kushiriki kutoa maamuzi na kupanga mipango ya maendeleo kutoka asilimia 78 mwaka 2015 hadi 95% mwaka 2020.	3.1.1 Kuimarisha utawala bora (uwazi/ukweli na uwajibikaji)	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuendesha semina kwa viongozi katika kata 23 juu ya majukumu yao kwa jamii.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano ya hadhara ya uhamasishaji katika kata 23 juu ya uwazi/ukweli na uwajibikaji.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano ya uhamasishaji katika kata 23 juu ya kupanga, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji na kutathimini miradi ya kiuchumi kwa makundi maalum.</li> <li>➤ Kuimarisha wawezeshaji wa Wilaya (TOTs) 75 kwa kuwapa semina rejea ya O&amp;OD.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya kupambana na kuzuia rushwa ngazi ya vijiji katika vijiji 77.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kupanda kwa kiwango cha ushiriki wa jamii kupanga mipango ya maendeleo kwa asilimia 17</li> </ul>
		3.1.2 Kuimarisha mfumo shirikishi katika kupanga na kusimamia miradi ya maendeleo.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mikutano ya hadhara ya kutoa maamuzi.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano ya uhamasishaji juu ya umuhimu wa jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye kata 23.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya uundaji wa Kamati /jumuiya mbalimbali za kusimamia</li> </ul>	

		<p>miradi kulingana na sera na sheria za sekta husika.</p> <ul style="list-style-type: none"><li>➤ Kuwasilisha na kujadili taarifa za maendeleo ya Kata 23 za kila robo mwaka.</li><li>➤ Kutoa elimu ya kuwezesha jamii kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika Kata 23.</li></ul>	
--	--	--	--

## JEDWALI NAMBA 6

### ENEO MUHIMU LA MATOKEO NA. 4: UZINGATIAJI WA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA JAMII

	LENGO MAHSUSI	MIKAKATI	SHUGHULI	VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI
4.1	Kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika Nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa kutoka asilimia 30 hadi 50.	4.1.1 Kuhamasisha jamii juu ya suala la jinsia kwa kushirikiana na AZISE.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Mafunzo kwa vikundi vya kijamii 360 juu ya uongozi na jinsia katika kata 23.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano juu ya suala la jinsia, ndoa na ushiriki katika uongozi katika Kata 23</li> <li>➤ Kutoa elimu juu masuala ya jinsia kwa vyombo vya kufanya maamuzi katika Kata 23.</li> <li>➤ Kutoa mafunzo kwa walimu 284 wa shule za msingi na sekondari juu ya jinsia na ushiriki katika uongozi.</li> <li>➤ Kuelimisha jamii juu ya sera, sheria ndogo na miongozo inayohusu masuala ya jinsia kwa Maafisa Watendaji na Mabaraza ya Kata.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano ya uhamasishaji katika kata kata 23 juu ya kuacha mila potofu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ongezeko la uzingatiaji wa usawa wa kijinsia kwa asilimia 20</li> </ul>
		4.1.2 Kuongeza kipato kwa kuimarisha vikundi vya wanawake vya kiuchumi kutoka 168 hadi 300 ifikapo mwaka 2020.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kusajili na kuwezesha vikundi 50 vya wanawake na vijana vya uzalishaji.</li> <li>➤ Kuendesha mafunzo kwa vikundi 300 vya uzalishaji mali vya wanawake kuhusu ujasiliamali, utunzaji kumbukumbu na usimamizi wa mikopo katika kata 23.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Vikundi 132 vya kiuchumi vya wanawake vimeongezeka.</li> </ul>

			<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuhamasisha vikundi vyatyanawake na vijana kujiunga na SACCOS.</li> <li>➤ Kufanya ufuutiliaji na usimamizi wa vikundi vyote vilivyosajiliwa vyatyanashuhuli za uzalishaji mara moja kwa robo mwaka.</li> </ul>	
4.2	Kuwezesha watoto walio kwenye mazingira hatarishi kutoka 2,600 hadi 4,000 ifikapo mwaka 2020	4.2.1 Kuhakikisha watoto walio kwenye mazingira hatarishi wanawezeshwa toka kwa jamii na wadau.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kubaini watoto walio kwenye mazingira hatarishi kwenye kata 23.</li> <li>➤ Kuelimisha kamati za watoto walio kwenye mazingira magumu za vijiji 77 juu ya majukumu yao.</li> <li>➤ Kufundisha wawezeshaji (50) TOTs) juu ya mbinu za matunzo ya watoto.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii juu ya kuchangia gharama za kuwatanza watoto walio katika mazingira hatarishi katika kata 23.</li> <li>➤ Kulipa ada za watoto 200 walio katika shule za sekondari kila mwaka.</li> <li>➤ Kutoa misaada zikiwemo balskeli na viungo bandia kwa watu 200 wenye ulemavu, kila mwaka.</li> <li>➤ Kuendesha mikutano ya kila robo mwaka ya wadau (AZISE) wanaolipia karo na mahitaji mengine wanafunzi.</li> </ul>	➤ Ongezeko la watoto 1,400 wanaowezeshwa.

**JEDWALI NAMBA 6**

**ENEO MUHIMU LA MATOKEO NA. 5: UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

	LENGO MAHSUSI	MIKAKATI	SHUGHULI	VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI
5.1	Kuungeza upandaji miche ya miti kutoka 1,500,000 kwa 2007 mpaka/ hadi 6,600,000 ifikapo mwaka 2020.	5.1.1 Uhamasishaji wa jamii kuanzisha na kuendeleza vitalu vyatya miche ya miti endelevu.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuunda makundi 117 ya uhamasishaji katika vijiji 77 na vitongoji 35 kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na vikundi vyatya jamii katika upandaji miti.</li> <li>➤ Kuhamasisha jamii kuungeza idadi ya vitalu kwa vijiji 77 na vitongoji 35kwa ajili ya kupanda miche 1,600,000 kila mwaka.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuwa na miti 5,100,000 iliyopandwa</li> </ul>
5.2	Kupunguza uvamizi na uharibifu wa misitu ya asili na hifadhi ya mazingira kutoka 70% hadi 30% ifikapo 2020.	5.2.1 Kushirikiana na wadau wote wanaoishi jirani na misitu ya asili na hifadhi ili kuzuia na kulinda uvunaji holela na uvamizi wa maeneo ya hifadhi .	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kutembelea, kukagua na kulinda mipaka ya misitu ya asili yote kama ilivyoelekezwa na sheria.</li> <li>➤ Kutambua na kutenga maeneo mapya 5 ya misitu kwa ajili ya kuhifadhiwa.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kupunguza uvamizi wa misitu ya asili na uharibifu wa mazingira kwa 40%</li> </ul>
		5.2.2 Uhamasishaji wa jamii ili kuacha uchomaji moto oyo.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kuunda kamati za kudhibiti uchomaji moto kwa kila kijiji.</li> </ul>	
		5.2.3 Uratibu wa wadau wote katika utunzaji na uboreshaji wa mazingira.	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kufanya/kuendesha mikutano kwa kata 23 juu ya utunzaji misitu ya asili, hifadhi na juu ya madhara ya uchomaji moto.</li> <li>➤ Kuendesha vikao vyatya kila robo kwenye kata 23 juu ya kuhifadhi, kulinda misitu na madhara ya uchomaji moto.</li> </ul>	

